**HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**
**KATA YA UYOGO**
**SHULE YA MSINGI NSUNGA**
**MTIHANI WA MUHULA WA PILI - 2025**
**SOMO: HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI DARASA LA TATU**

**JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………………………………….**

**MUDA: 1:00**

## Sehemu: A (Alama 20)

1.**Chagua herufi ya jibu sahihi katika kipengele cha i-v na kuandika herufi yake katika kisanduku.**

(i) Makundi maalumu ya watu ni wazee, watoto na________(A) Walemavu(B) Wasomi(C) Viongozi(D) Matajiri ( )

(ii)Jambo linalo mlazimu mtu kulifanya au kulitimiza huitwa_______(A) Haki (B) Lazima (C) Wajibu (D) Utendaji ( )

(iii)Bainisha njia mojawapo ya kujenga urafiki shuleni._______(A) Kugombana (B) Kucheza pamoja (C) Kupeana pesa (D) Kupigiana simu ( )

(iv)Elimu inayohusu matukio yanayotokea nchini Tanzania tangu mwanzo hadi sasa katika maisha ya watu huitwa___________(A) Historia ya kigeni (B) Historia ya Tanzania (C) Historia na maadili (D) Kumbukumbu ( )

(v)Familia au jamaa zenye uhusiano wa damu ni_____(A) Koo(B) Kabila(C) Dini(D)Mila **( )**

(vi)Vifuatavyo ni vitendo vya kimaadili isipokuwa_______(A)Kusaidia wazee (B)Kusalimiana (C)Kupigana (D)Kuheshimiana ( )

(vii)Masalia ya fuvu la binadamu wa kale yaligunduliwa mwaka______(A)1961 (B)1959 (C)1962 (D)1970 ( )

(viii)Nyavu,ndoano na mitumbwi ni vifaa vya asili vya________(A)Usafi (B)Uwindaji (C)Biashara (D) Uvuvi ( )

(ix)Kiongozi mkuu wa familia ni________(A)Kaka (B)Dada (C)Baba (D)Babu ( )

(x)Kumtibu mgonjwa kwa kumgubika ni maarifa na ujuzi wa_________(A)Kiufundi (B)Kiasili (C)Kisasa (D)Kidijitali

( )

**2.Oanisha maneno ya fungu A na B ili kuleta maana kamili.**

| | FUNGU A | JIBU | | FUNGU B |
|---|---|---|---|---|
| i. | Utumwa | | A | Masalia ya fuvu la binadamu wa kale |
| ii. | Alama ya pundamilia | | B | Viungo vya chakula vilivyoletwa na wageni |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| iii. | Mlima Kilimanjaro | | C | Kutawaliwa na watu wageni |
| iv. | Iliki,mdalasini, karafuu,pilipili manga | | D | Huchorwa barabarani kwa rangi nyeupe |
| v. | Olduvai, Arusha | | E | Mlima mrefu barani Afrika |

**3.Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno kwenye kisanduku**

| **Matendo ya kusalimiana, Mjomba, Mwalimu mkuu, Dini, Magofu** |
|---|

(i)Imani inayohusisha kuwepo kwa Mungu au miungu_____________________

(ii)Kaka wa mama yako unamwitaje ?______________________

(iii)Mabaki ya majengo ya kale yanayoonekana ______________________

(iv)Kiongozi mkuu katika shule ni _____________________

(v)Kubusu mkono, kupiga goti, kushika kichwa ________________________

**Sehemu B: (Alama 20)**

**4. Weka alama ya vema (√) kwenye kisanduku kwa kubainisha matendo ya haki na wajibu wa watoto**

| | **MATENDO** | **HAKI** | **WAJIBU** |
|---|---|---|---|
| i | Kulindwa | | |
| ii | Kushiriki kufanya maamuzi | | |
| iii | Kupata nafasi ya kucheza | | |
| iv | Kufanya kazi kwa bidii | | |
| v | Kutobaguliwa kwa njia yoyote | | |

**5.Jaza nafasi zilizo achwa wazi**

i.__________________ni mwenendo au utendaji uliokubalika katika jamii.

ii. Maeneo yanayotumiwa kuhifadhi vitu vyenye historia na urithi wa kiasili huitwa___________

iii.________________ni hali ya uzima na kuwa na siha njema.

iv.____________________mbolea inayotokana na kinyesi cha wanyama.

v. Chakula cha asili chenye mchanganyiko wa mahindi na maharage huitwa_________________

**Sehemu C: (Alama 10)**

**6.Soma kwa makini kifungu cha habari kisha jibu maswali.**

Kilwa mkoani Lindi ina mabaki ya magofu ya mji, majengo na biashara ya utumwa. Kilwa kisiwani ndio mji uliokuwa kituo muhimu na kikubwa wakati wa biashara zilizofanywa na watu kutoka mashariki ya kati.Kilwa kuna masalia ya jengo la mfalme wa Kilwa liitwalo Husuni kubwa Jumba hili lilikuwa Ikulu ya Sultani wa Kilwa .

**Maswali**

i.Kilwa hupatikana mkoa gani ?____________________________________

ii.Biashara gani kubwa ilifanyika Kilwa ?______________________________

iii.Biashara iliyofanyika Kilwa ilikuwa baina ya watu wa Kilwa na___________________

iv.Jengo la Ikulu la Kilwa liliitwaje ?____________________________

v.Jumba la Kilwa lilikuwa ikulu ya nani ?________________________